**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dar es Salaam***
***21 Julai, 2026***

**YAH: UTEUZI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na Wenyeviti wa Bodi. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, walioteuliwa ni:-

(i) Bw. Salum Nassor Mnuna ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA);

(ii) Prof. Esron Daniel Karimuribo ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI); na

(iii) Bw. Paul Peter Olekashe ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI).

Shaaban Kissu
Kny. Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu